

**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU
HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA KWENYE MKUTANO NA VIJANA
MWANZA, TAREHE 15 JUNI, 2021**

*Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi
ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira
na Wenye Ulemavu;*

Waheshimiwa Mawaziri wengine mliopo;

*Ndugu Christine Mndeme, Naibu Katibu Mkuu
wa CCM Taifa pamoja na Viongozi wengine
wa Vyama vya Siasa mliopo;*

*Ndugu Kheri James, Mwenyekiti wa Vijana
wa CCM Taifa;*

*Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel,
Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;*

Waheshimiwa Wabunge mliopo;

Waheshimiwa Mameya na Madiwani mliopo;

Ndugu Makatibu Wakuu mliopo;

Viongozi wa Dini na Wazee wa Mwanza;

Viongozi wengine wa Serikali mliopo;

Makundi mbalimbali ya Vijana mliopo;

Ndugu Wasanii, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana;

“VIJANA OYEEE”

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA**

Awali ya yote, napenda kuungana na wote
walionitangulia kuzungumza katika kumshukuru

Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na kutuwezesha kufika hapa. Niwashukuru pia Ofisi ya Waziri wa Mkuu, Uongozi wa Mkoa wa Mwanza pamoja na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kwa maandalizi na uratibu mzuri wa Mkutano huu.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru vijana kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu Shinyanga, Geita) kwa kujitokeza kwa wingi katika Mkutano huu. Kwa kweli mmetia fora; na kusema kweli, sikutarajia kukuta umma mkubwa kiasi hiki. Hii inaonesha kuwa mnaiunga mkono na mko pamoja na Serikali.

Ndugu Vijana na Watanzania mnaonisikiliza;

Sio siri kuwa vijana ni kundi muhimu katika taifa lolote. Hii ni kwa sababu, kitakwimu, vijana wapo wengi. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, katika kila **watu 10** nchini, **wanne** ni vijana ambao wana umri kati ya **miaka 15** na **35**. Hivyo, kwa takwimu za sasa, nchi yetu inakadiriwa kuwa na vijana wapatao **milioni 21**.

Ukiachilia mbali takwimu hizo, vijana ni nguvu kazi ya taifa; ni walinzi wa taifa; ni watu wenye ubunifu, wana uthubutu, ni wajasiri na ndiyo waliobeba maono na matarajio ya Taifa kwa sasa na siku zijazo. Kwa maneno mengine, uhai, usalama, maendeleo na ustawi wa taifa

lolote duniani unawategemea vijana. Hakuna taifa linaloweza kusonga mbele bila kutegemea vijana wake.

Waheshimiwa Viongozi;

Ndugu Vijana na Wananchi mnaonisikiliza;

Pamoja na ukweli huo, kundi hili la vijana linakabiliwa na changamoto nyingi. Baadhi ya wazungumzaji walionitangulia wametaja changamoto zinazowakabili vijana nchini; lakini na mimi naomba nizitaje na kueleza hatua zinazochukuliwa na Serikali kuzitatua.

Changamoto ya *kwanza* ambayo naamini ni kubwa zaidi ni **tatizo la ajira**. Nchi yetu, kama ilivyo kwa nchi zote duniani, inakabiliwa na uhaba mkubwa wa ajira. Hata hivyo, tatizo hili linawakabili zaidi vijana, ambapo, kwa

wastani, **asilimia 11.4** ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi hawana ajira.

Katika kutatua tatizo hili, Serikali yetu inajitahidi kuchukua hatua mbalimbali za kulipunguza. Kwanza, kwa kuendelea kuajiri. Kama mnavyofahamu, Serikali ndiyo mwajiri mkuu hapa nchini. Kumekuwa kukitolewa matangazo ya ajira kwenye sekta mbalimbali, ambapo vijana wengi wamekuwa wakijitokeza kuziomba. Hata hivyo, kutokana na uchache wa nafasi, wengi wao wamekuwa hawafanikiwi. Kwa mfano, hivi karibuni, tumetangaza nafasi za ajira katika kada za ualimu na afya zipatazo 9,000; ambapo walioomba ni zaidi ya 90,000. Hivyo, ni wazi kuwa wengi hawatofanikiwa. Lakini hii inatokana na ukweli kwamba, ajira kwenye sekta ya umma

zinaendana na uwezo wa nchi na Serikali kiuchumi na kulipa mishahara.

Sambamba na kuajiri moja kwa moja, Serikali inatengeneza fursa za ajira kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa Reli ya Kisasa; Bwawa la Umeme; barabara; madaraja; ukarabati na ujenzi wa meli mpya; viwanja vya ndege; na hivi karibuni tutaanza kutekeleza Mradi wa Bomba la Mafuta. Hizi zote ni fursa za ajira.

Njia nyingine inayotumiwa na Serikali ni kutengeneza mazingira mazuri ya kukuza sekta binafsi ili ijenge viwanda na kuanzisha biashara mbalimbali zitakazotoa ajira kwa wananchi. Vilevile, Serikali inatengeneza mazingira ya

vijana kujiajiri wenyewe kwa kufuta tozo kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Serikali pia imerahisisha taratibu za biashara, ikiwemo kutoa leseni kwa njia ya mtandao (*online registration*) na kufuta tozo na kodi za kero za OSHA, Zimamoto, n.k. Kwenye madini tumefuta tozo na kodi mbalimbali na kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo yenye ukubwa wa **hekta 38,567**.

Maeneo mengine ambako tumeboresha mazingira ili kuongeza fursa za ajira ni kwenye sekta ya utalii, ambako tumeanzisha Hifadhi tano mpya za Taifa na kununua ndege mpya 11. Tumepunguza pia ada ya leseni ya biashara ya utalii kwa wakala wa kusafirisha watalii yenye idadi ya magari chini ya manne kutoka **Dola za Kimarekani 2,000** hadi **Dola za Marekani 500**. Kwenye TEHAMA, Serikali

imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye Mkongo wa Taifa na kujenga Kituo cha Kisasa cha Kutunza Taarifa (yaani **Data Centre**). Hii ni fursa kwa Watanzania kunufaika na uchumi wa kimtandao (*digital economy*) kupata ajira. Serikali pia imeboresha upatikanaji wa umeme. Hii pia ni imeongeza fursa kwa vijana kupata ajira na kujiinua kiuchumi.

Eneo jingine ni michezo, sanaa na utamaduni. Kama mnavyofahamu, kwenye miaka ya hivi karibuni, sekta hii imekuwa ikikua kwa kasi na kutoa ajira nyingi, hususan kupitia michezo mbalimbali, muziki, filamu. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali kuikuza na kuimarisha sekta hii ili iendelee kutengeneza fursa za ajira ni kuimarisha usimamizi wa hati miliki za wasanii. Na

katika hilo, nataka niarifu kuwa kuanzia mwezi Disemba 2021, wasanii wataanza kulipwa mrabaha yao kutokana na kazi zinatumiwa kwenye runinga, redioni na mitandaoni.

Tumeanzisha pia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ili kusaidia kuziandaa Timu zetu za Taifa; na kama mlivyosikia, kwenye Mwaka ujayo wa Fedha, tumefuta VAT ya nyasi bandia ili kuboresha viwanja vyetu vya michezo. Na hapa nina maneno kidogo kwa Chama changu (CCM). Kama mnavyofahamu, viwanja vingi vinamilikiwa na CCM. Hata hivyo, hali ya viwanja hivyo hairidhishi. Hivyo basi, kwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM yupo hapa, nakuagiza kuandaa programu ya kuviboresha

viwanja hivyo. Kama hamna uwezo, tafuteni wawekezaji, mshirikiane nao.

Waheshimiwa Viongozi;

Ndugu Vijana na Wananchi mnaonisikiliza;

Ukiachilia mbali tatizo la ajira kwa vijana, changamoto nyingine inahusu **elimu na ukosefu wa ujuzi**. Katika kushughulikia suala hili la elimu na ujuzi, Serikali imechukua hatua mbalimbali. Kwanza, Serikali inatoa elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari; pili, tumeongeza idadi ya shule za sekondari pamoja na mikopo ya elimu ya juu. Mathalan, kwenye Mwaka ujao wa Fedha tumetenga **shilingi bilioni 500** ambazo zitawanufaisha wanafunzi **160,000** kutoka **shilingi bilioni**

464 za mwaka 2020/2021 ambazo zimewanufaisha wanafunzi **149,472**.

Kuhusu ujuzi, hatua mbalimbali zinachukuliwa, ikiwemo kujenga vyuo vya ufundi kwenye Wilaya na Mikoa. Aidha, tumeanzisha vituo mahiri vya mafunzo kwa taasisi za elimu ili kuzalisha vijana wenye uwezo unaohitajika, ambapo kiasi cha **Dola za Marekani milioni 75** kimepangwa kutumika. Vituo hivyo vya umahiri ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itakayoboea katika masuala ya TEHAMA na Taasisi ya Teknolojia ya hapa Mwanza itaboea kwenye masuala ya Ngozi; na Chuo chetu cha Taifa cha Usafirishaji kitaboea katika taaluma za anga wakati Chuo cha Ufundi Arusha kitaboea katika nishati jadifu. Aidha, mtakumbuka kuwa, juzi wakati

nikizindua Mtambo wa Dhahabu nilimwelekeza Waziri wa Madini kukiimarisha Kituo cha Jemolojia Tanzania (*Tanzania Gemmological Centre - TGC*) kilichopo Arusha ambacho kinatoa mafunzo ya ngazi ya cheti na diploma katika fani ya teknolojia ya madini na usonara, utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji na utengenezaji wa mapambo na urembo. Kwenye masuala ya sanaa na utamaduni, tutakiimarisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Na hapa nataka pia kumwagiza Waziri wa Michezo, pamoja na azma ya Wizara ya kujenga Sport Arena, anzeni pia kufikiria kujenga vituo vya michezo (yaani *academy*) katika mikoa ili kukuza vipaji.

Vilevile, Serikali tangu mwaka 2016/2017 inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi ambapo mpaka sasa

vijana **65,598** wamewezeshwa kupata ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa katika fani mbalimbali katika sekta za utalii na ukarimu (tourism and hospitality), ujenzi, TEHAMA, kilimo biashara, ushonaji nguo na viwanda. Hivi sasa, vijana wengine **14,440** wanaendelea na mafunzo ya kukuza mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo na Ufundi Stadi. Sambamba na hayo, mtakumbuka kuwa, wakati nikilihutubia Bunge, niliahidi kuwa Serikali itafanya mapitio ya mitaala yetu ili elimu tunayoitoa iwawezeshe wahitimu kupata ujuzi na stadi za kazi.

Ndugu Vijana na Ndugu Wananchi;

Ukosefu wa mitaji ni changamoto nyingine kubwa inayowakabili vijana. Tatizo hili linatokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kukosa vigezo vya kupata mikopo

kwenye taasisi za fedha, kukosa taarifa za wapi wanaweza kupata mikopo; lakini pia vijana wenyewe kushindwa kutumia fursa zilizopo.

Katika kutatua tatizo hilo la mitaji, Serikali imeanzisha Mifuko na Programu mbalimbali za kuwawezesha vijana, ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ambao mpaka sasa umetoa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 5.43** ambayo imewanufaisha vijana **6,293**; Programu ya Ujasiriamali kwa Vijana wa Elimu ya Juu ambapo vijana **8,736** wamenufaika na ruzuku au mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 5.6**. Sambamba na hayo, kama mnavyofahamu, Serikali, kupitia **asilimia 10** ya mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini, inatoa mikopo kwa vijana (**asilimia 4**), wanawake (**asilimia 4**) na watu wenye

ulemavu (**asilimia 2**). Kwa bahati nzuri vijana wapo kwenye makundi yote haya; na nimeambiwa katika Mkoa huu wa Mwanza kiasi cha **shilingi bilioni 5.679** kimetolewa kwa wanufaika **2,112**.

Pamoja na jitihada hizo za kuwapatia vijana mikopo, natambua kuwa tatizo la mitaji kwa vijana bado ni kubwa. Na katika hilo, nataka kutumia fursa hii kuarifu kuwa hivi majuzi nilifanya mazungumzo na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dkt. Adesina, ambaye ameahidi kushirikiana na Serikali yetu kuongeza vyuo vya ufundi na stadi za kazi pamoja na kuanzisha Benki ya Ujasiriamali hapa nchini. Kuanzishwa kwa Benki hiyo kutasaidia kutatua tatizo la mitaji kwa vijana.

Ndugu Vijana na Ndugu Wananchi;

Changamoto ya nne inayowasibu vijana ni kukosa maeneo ya uhakika na mazuri ya kuendesha shughuli zao. Na hapa nawazungumzia zaidi wamachinga, mama lishe pamoja na wajasiriamali wengine wadogo. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imejenga masoko na stendi ili kuwapatia vijana maeneo ya kuendesha shughuli zao. Aidha, Serikali imezielekeza halmashauri zote nchini kutenga maeneo ya kuwawezesha vijana kuendesha shughuli zao za maendeleo. Na hapa nataka niseme, hivi majuzi niliona kupitia runinga, pale Morogoro; vijana wametengewa maeneo mbali na mjini tena bila kuwekewa miundombinu muhimu. Hii ikafanya vijana wale warudi kwenye maeneo ya zamani. Viongozi wa Wilaya, badala ya kushughulikia changamoto zilizosababisha vijana wale

kurudi kwenye maeneo ya zamani, waliwatuma mgambo kwenda kuwapiga na kuwanyang'anya mali zao. Kwa kweli, hii ilinisikitisha sana; na kwa sababu hiyo, natamka nitamke kwamba, kuanzia leo Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Morogoro nimewaondoa kwa kushindwa kushughulikia suala hilo vizuri.

Sanjari na kutenga maeneo, kama mnavyofahamu, Serikali imetoa Vitambulisho Maalum kwa wajasiriamali wadogo ili kuwawezesha kuendesha shughuli zao bila kubughudhiwa. Hata hivyo, natambua kwamba kilio kikubwa cha wajasiriamali wadogo ni kutaka vitambulisho hivyo viboreshwe. Tumeanza kufanyia kazi suala hilo ili Kitambulisho hicho kiwe na taarifa nyingi za Mjasiriamali

husika zitakazomwezesha kutambulika, ikiwemo kwenye taasisi za fedha. Lakini, nitumie fursa hii kuwasihi sana wanufaika wa vitambulisho hivyo, kutokubali kutumiwa na matajiri (wenye maduka) kukwepa kodi. Tumieni fursa mliyopewa na Serikali kukuza biashara zenu ili siku moja nanyi muweze kukua ama kuhitimu kutoka ujasiriamali mdogo na kuwa wafanyabiashara wa kati hatimaye kuwa wakubwa. Serikali itashirikiana nanyi katika kuandaa Mpango Kabambe wa kurasimisha biashara zenu na kuwawezesha kuhitimu na kukua. Tunataka na nyie siku moja mchangie maendeleo ya taifa letu kupitia kodi.

Ndugu Vijana na Ndugu Wananchi;

Kama nilivyosema awali, sehemu kubwa ya Watanzania ni vijana, ambapo wengi wamezaliwa baada ya

Uhuru ama Muungano. Kwa kutambua hilo, tumejitahidi kuteua kundi hilo kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi (Baraza la Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Ma-RAS, na hivi karibu *kuna mkeka/nitateua* Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi ambapo wengi watakuwa vijana). Hii ni fursa kubwa kwenu vijana, ingawa baadhi yenu tunapowateua mnatuangusha. Vyama vya Siasa pia vimeweka mifumo inayoweza vijana kuingia kwenye Bunge. Ukiachilia wale wanaoingia Bungeni kupitia Kundi la Vijana, wabunge wengi wa kuchaguliwa hivi sasa ni vijana. Hata kule Zanzibar hali iko vivyo hivyo. Rais wa Zanzibar ni Kijana; lakini pia kuna Mawaziri na Wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi ambao ni vijana. Kwenye sekta binafsi nako hali iko vivyo hivyo; wengi ni vijana. Hii inatoa taswira

kwamba kwa sasa nchi yetu inaongozwa na vijana wakaishirikiana na wazee wachache.

Sasa vijana waliopata nafasi hizo wajiulize, je utendaji wao wa kazi ukoje, wana ufanisi wa kutosha na uzalendo wao ukoje. Lakini, swali jingine la kujiuliza ni kwamba, hapa tulipo leo kuna vijana wa rika, jinsia, elimu na itikadi mbalimbali; je ni wapi mnakutana? Mkitoka hapa, mnakwenda wapi kama vijana kujadili masuala yenu na kuweka ajenda za kitaifa bila kujali jinsia, elimu na itikadi zenu za vyama? Na hapa ndipo inakuja ile hoja iliyowasilishwa na mmoja wa wabunge kuhusu Baraza la Vijana, ambalo limesemwa siku nyingi lakini halijaundwa. Tutakwenda kuangalia kwa undani kwa nini Baraza hilo

halijaundwa na tuone namna ya kuliunda ili litumike kuwa jukwaa la kuwakutanisha vijana wa Tanzania kujadili mambo yenu na ajenda nyingine za kitaifa.

Hata hivyo napenda niseme, ingawa ni kweli kwamba Baraza la Vijana halipo, lakini Mabaraza ama Jumuiya za Vijana za Vyama zipo. Sasa tujiulize Mabaraza hayo ni lini yanakutana kujadili masuala ya kitaifa na kutoa mapendekezo? Kubwa ninaloliona mimi ni kwa Mabaraza na Jumuiya hizo kutumika na wagombea wakati wa Uchaguzi na sio kujadili masuala yanayohusu vijana. Hivyo basi, naziomba Jumuiya za Vijana za Vyama kubadilika na kuanza kujadili masuala yenye maslahi kwa vijana kama Katiba zenu zinavyoelekeza. Na kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti wa CCM, naitaka Jumuiya ya Vijana ya CCM

kuanza kujipanga ili kubeba ajenda za kitaifa. Mjipange kuangalia yanayotokea nchini na kutoa mapendekezo yenu. Nina uhakika, ninyi mkianza, Jumuiya nyingine zitafuata.

Lakini sambamba na hayo niliyoeleza, lipo suala jingine linalohusu ushiriki wa vijana kwenye majukwaa ya kikanda na kimataifa (EAC, SADC, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa). Je vijana wa Tanzania mnashiriki vipi; ni akina nani wana wawakilisha na wanapatikanaje. Ninafahamu yapo mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayofadhiliwa kushiriki mikutano hiyo, lakini tujiulize mrejesho wanaupeleka kwa nani? Hili nalo vijana mnatakiwa kulifanyia kazi; vinginevyo mtaendelea kunyang'anywa haki zenu.

Sambamba na hayo, **Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana** ya sasa ni ya muda mrefu. Imetungwa mwaka 2007. Tangu wakati huo, mabadiliko makubwa yametokea hapa nchini na duniani kwa ujumla ambayo yameathiri Sera ya Vijana. Swali langu ni kwamba, ni lini vijana mlikaa kuipitia Sera hiyo na kutoa mapendekezo ya kuiboresha. Mfano, wakati Sera inapitishwa mwaka 2007 suala la uchumi mtandao (*digital economy*) halikufikiriwa kabisa kama linaweza kuwa chombo muhimu cha maendeleo hapa nchini na duniani kwa ujumla. Hivi sasa, suala la uchumi mtandao ni nguzo muhimu ya maendeleo duniani. Mfano mwingine ni kwenye afya. Tangu Sera imepitishwa, masuala mengi yamebadilika ambayo ingefaa yafanyiwe

marekebisho kwa kuingizwa ni Sera mpya. Hii ni mifano michache tu.

Ndugu Vijana na Ndugu Wananchi;

Changamoto nyingine ni pamoja na athari za **UKIMWI** pamoja na **Dawa za Kulevya**. Takwimu zinaonesha kuwa maambukizi mengi mapya yanatokea kwa vijana. Aidha, vijana ni waathirika wakubwa wa dawa za kulevya. Matatizo mengine ni rushwa. Kama mnavyofahamu, vijana ndio watoa huduma na wapokea huduma mbalimbali. Hivyo, tatizo la rushwa linawahusu.

Serikali inajitahidi kushughulikia masuala hayo. Mathalan, kuhusu UKIMWI tunaendelea kutoa elimu ili kuwaepusha vijana dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa

UKIMWI. Aidha, kuhusu rushwa na dawa za kulevya, nyote ni mashahidi kuwa kwenye miaka mitano iliyopita, nchi yetu imefanikiwa sana katika kupiga vita rushwa na kudhibiti uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Na hii imethibitishwa na Ripoti mbalimbali za Taasisi za Kimataifa. Mfano, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), limeipongeza nchi yetu kwa kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya kwa **asilimia 90**. Zaidi ya hapo, nchi yetu imesifiwa kwa kupiga vita rushwa. Wajibu wenu vijana ni kuhakikisha mnayalinda mafanikio haya.

Ndugu Vijana, Mabibi na Mabwana;

Kwa ujumla, Serikali imejitahidi sana kuwawezesha vijana. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 -

2025, imeielekeza Serikali kuendelea kushughulikia masuala ya vijana, ikiwemo kutengeneza fursa za ajira zipatazo **milioni 8**. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, ni ukweli usiopingika kuwa, jitihada za Serikali pekee haziwezi kumaliza matatizo ya vijana. Ni lazima ninyi vijana wenyewe muwe mstari wa mbele. Na katika hilo, napenda kutumia fursa hii kutoa wito ufuatao kwa vijana.

Kwanza kabisa, vijana hamna budi kutumia fursa zilizopo. Nchi yetu inazo fursa nyingi. Na moja ya fursa kubwa tuliyonayo ni kwenye kilimo. Nchi yetu ina takriban **hekta milioni 29** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hii ni fursa kubwa kwa vijana. Na hapa simaanishi kwamba lazima mkalime. Kama mnavyofahamu, kilimo kina mnyonyoro mrefu (usambazi pembejeo na zana, huduma za

ugani, uhifadhi, biashara na masoko, usafirishaji, usindikaji mazao, n.k.). Fursa nyingine ni kwenye mifugo, ambapo tunashika nafasi ya pili Barani Afrika kwa idadi ya mifugo. Aidha, Tanzania ina eneo la maji lenye ukubwa wa kilometa za mraba **397,937**, ambayo ni sawa na **asilimia 41.1** ya eneo lote la Tanzania; ambalo linafaa kwa shughuli za uvuvi. Na kama nilivyosema awali, fursa nyingine ipo kwenye uchumi wa mtandao, ambapo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika kujenga Mkongo wa Taifa na Kituo cha Kanzidata.

Hivyo, kinachohitajika kwa vijana ni kujiamini na kutumia fursa hizo. Nitumie fursa hii kuwapongeza baadhi ya vijana wanaotumia mitandao kujipatia vipato (kufanya biashara, kuanzisha televisheni na radio). Lakini, kupitia

mitandao, wapo vijana wanaoitumia vibaya kulaumu, kushutumu, kukashfu bila ushahidi au kutoa mapendekezo.

Sambamba na hilo, nawasihi sana vijana wangu mshirikiane. *“Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”*. Wakati mwingine, vijana mnashindwa kufikia malengo yenu kwa vile kila mmoja anafanya mambo peke yake. Mkishirikiana itakuwa rahisi kwa Serikali kuwasaidia. Na katika hilo, natambua kuwa kuna vijana wajasiriamali na wabunifu ambao wameanzisha biashara (*startups*). Nataka kutumia fursa hii kuwaahidi kuwapa ushirikiano kupitia umoja wenu wa *Tanzania Start-up Association (TSA)*. Nirudie tena kuwahamasisha vijana wengine nao kuungana ili rahisi kwa Serikali kuwawezesha. Kumbukeni ule usemi

usemao “Ukitaka kwenda haraka nenda peke yako; lakini ukitaka kwenda mbali nenda na wenzako”.

*Waheshimiwa Viongozi,
Ndugu Vijana;
Mabibi na Mabwana;*

Nimeeleza mengi. Lakini, kabla sijahitimisha, kama mnavyofahamu, leo nahitimisha ziara yangu hapa Mkoa wa Mwanza. Nimekuwepo hapa kwa takriban siku tatu. Nimepata fursa ya kukagua miradi ya maendeleo na kuwasalimu wananchi. Nimefurahi miradi mingi inaendelea vizuri. Nitumie fursa hii kuwataka Viongozi wa Mkoa wa Mwanza kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na viwango.

Nawahimiza pia wana-Mwanza kutumia fursa mbalimbali zinaletwa na Serikali kwenye Mkoa wenu.

Sambamba na hiyo, wakati wa ziara hii nimepokea kero mbalimbali za wananchi, ambapo kubwa ni upatikanaji wa huduma za maji, umeme, vituo vya afya, upungufu wa watumishi wa kada za ualimu na afya na pia ubovu wa barabara, hususan vijijini. Napenda kurudia tena ahadi yangu kuwa Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji, umeme na maji vijijini. Lakini, kuhusu maji, napenda nirudie nilichokisema jana nikiwa Misungwi kuwa, maji ni rasilimali adimu ambayo inazidi kupungua kila miaka inavyopita kutokana na uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa idadi ya watu. Wakati tunapata uhuru,

wastani wa mtu kupata maji ilikuwa **mita za ujazo 12,600**; hivi sasa wastani ni **mita za ujazo 2,250**.

Hivyo basi, hatuna budi kulinda na kutunza vyanzo vyetu vya maji kwa kuacha kuchoma misitu, kukata miti hovyoyo na pia kulisha mifugo karibu na vyanzo vya maji. Aidha, nawahimiza kupanda miti. Kuna usemi unasema *“ukiyaudhi mazingira, nayo yatakuadhibu mpaka pale ukarudisha urafiki nayo”*.

Nihitimishe kwa kurudia kuwashukuru Viongozi wote wa Serikali na Chama wa Mkoa wa Mwanza kwa maandalizi mazuri ya ziara hii. Vilevile, navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimeendelea

kutulinda na kuhakikisha usalama wetu. Nazishukuru taasisi ambazo tulipata fursa ya kwenda kuzindua, kukagua na kuweka mawe ya misingi ya miradi yao. Nawashukuru pia Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini ambao tumekuwa pamoja katika ziara yote. Nawashukuru wana-Habari na Vijana wetu wa Skauti, Wasanii na Madereva; wote nawashukuru.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, narudia kuwashukuru wana-Mwanza kwa ukarimu wenu mkubwa mlionesha kwangu na ujumbe nilioambatana nao. Naondoka Mwanza nikiwa mwenye furaha sana. Na nataka niseme kuwa baadhi ya wasaidizi wangu waliniomba

niongeze siku kidogo. Hata hivyo, kutokana na majukumu imeshindikana; lakini naahidi *penye majaaliwa* nitakuja tena Mwanza kutembelea maeneo ambayo sikufanikiwa kufika (Kwimba, Magu, Sengerema, Ukerewe). Lakini kwa leo itoshe tu kusema **“Wabheja sana wana-Mwanza”**.

Baada ya kusema hayo, Mungu Wabariki Vijana!

Mungu Wabariki wana-Mwanza!

*Narudia Kuwasalimu kwa Jina la Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania!*

“Ahsanteni sana kwa kunisikiliza”